HALMASHAURI YA MJI KASULU

(*Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Mji****)***

Simu/Fax 255-028-2810355 S.L.P. 475.

Mhe: Mwenyekiti

Mkutano wa Baraza la Madiwani

MJI- KASALU.

YAH: TAARIFA YA KAMATI YA MIPANGO MIJI, UJENZI NA MAZIINGIRA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI-MACHI (2016/2017).

Katika kipindi cha mwezi Januari-Machi 2017, kamati ya Mipango Miji,Ujenzi na Mazingira ilitekeleza shughuli zifuatazo kama zinavyoonekana kwenya hizi Idara zifuatazo.

- Idara ya Ujenzi
- Idara ya Ardhi na Mipango Miji
- Idara ya Usafi na Mazingira

Taarifa kamili imeambatanishwa.

Naomba kuwasilisha.

Mh.Emmanuel Kisunzu

Mwenyekiti

Kamati ya Mipango Miji,Ujenzi na Mazingira

Halmashauri ya Mji- KASULU

Mh. Mwenyekiti,

Katika kipindi cha robo ya nne yaani April –Juni 2016, Kamati ilipitia taarifa ya utendeji wa Idara ya Ujenzi. Katika kipindi hicho Idara ya Halmashauri kupitia Idara ya Ujenzi imeendelea kutekeleza miradi ya matengenezo ya barabara kwa bajeti ya mwaka 2015/2016. Hata hivyo kutokana na kuchelewa kwa fedha kutoka OR-TAMISEMI, Halmashauri imechelewesha kuanza kutekeleza kwa kazi hizo kwa wazabuni wawili kati ya wanne kwa kuwa katika kipindi hicho Halmashauriilikuwa imepokea ilikuwa imepokea Tsh 74,730,199.33 tu kutoka OR-TAMISEMI kati ya Tsh 625,980,000.00 ambazo zilikuwa zimekasimiwa katika bajeti ya mwaka huo 2015/2016.

Halmashauri pia imetoa taarifa ya kupungua kwa bajeti ya matengenezo ya barabara kwa mwaka 2015/2016 kutoka Sh 625, 980,000.00 hadi Sh. 525,755,000.00. Upungufu huo wa bajeti amabo ni sawa na 16% umeathiri pia hali ya utekelezaji katika maeneo mbalimbali ya utekelezaji katika kata zetu.

Aidha Halmashauri kupitia Idara ya Ujenzi kwa kushirikiana na idara ya Elimu Sekondari imekamilisha miradi miwili ya ujenzi wa nyumba ya watumishi katika shule ya Sekondari Murfiti '6 in 1' mradi uliogharimu jumla ya Tsh 150,000,000.00 na wa ujenzi wa choo chenye matundu 8 na tanki la kuvunia maji katika Sekondari ya Kasange umegharimu jumla ya Tsh 36,000,000.00

Katika robo hii ya nne Idara pia imeanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba ya watumishi 6 in 1, vyumba vine vya madarasa, choo cha cha matundu nane cha wanafunzi, choo vha cha matundu mawili cha watumishi na tank la kuvunia na kuhifadhia maji ya mvua katika shule ya sekondari Muhunga mradi huo pia unakadiriwa utatumia jumla ya Tsh 301,635,000.00 mpaka utakapokamilika. Mradi huu upo katika hatua za upauaji na umaliziaji.

Halmashuri kupitia Idara pia imeendelea kusimamia na kutoa elimu juu ya majenzi mjini kwa kuzingatia sheria za ujenzi mjini

IDARA YA ARDHI NA MIPANGO MIJI.

TAARIFA ZA KAZI ZILIZOFANYWA ROBO YA TATU, JANUARI – MACHI 2017.

3. Kitengo cha Mipango miji.

NA.	MRADI/SHUGHULI	UTEKELEZAJI	MAELEZO
1.	Kufanya uhamasishaji wa kuandaa mchoro wa mpango mji eneo la mudyanda	Taarifa za maeneo ya watu 306 wa eneo husika zimechukuliwa	Kazi inaendelea.(ilisimama kutokana na wananchi wengi kwenda kwenye shughuli za kilimo)
2.	Kuidhinisha vibali vya ujenzi 10.	Jumla ya ramani 10 zilizowasilishwa ofisini zimeidhinishwa kutokana na matakwa mipango miji kwenye maeneo husika.	Kazi hii ni endelevu kulingana na maombi yanavyowasilishwa.
3.	Kutambua watu ambao mchoro wa upimaji umefika kwenye maeneo yao.	Jumla ya watu 68 wametambuliwa pamoja na ukubwa wa maeneo yao.	Zoezi hili ni endelevu kulingana na mahitaji ya wananchi wa Mji wa Kasulu

2. Kitengo cha Upimaji na Ramani

NA	MRADI/SHUGHULI	HATUA YA UTEKELEZAJI	MAELEZO
1.	Kurudishia mipaka iliyopotea kwa viwanja vya 23.	Jumla ya viwanja 23 vimerudishiwa mipaka na kufanyiwa mahesabu (coordination).	Wateja walihudumiwa kwa kadri walivyofika ofisini.
2.	Upimaji wa viwanja 1013 eneo la kabanga	Jumla ya viwanja 1013 mahesabu yake yamekamilika (coordinated).	Ramani za upimaji zimekamilika na kurejeshwa halmashauri ya mji.
3	Upimaji wa viwanja katika mji wa Kasulu	Jumla ya viwanja 7 vimepimwa (kata ya Murusi 2, kata ya Mwilamvya 3 na kata ya Kumsenga 2) na mahesabu yake yamekamilika.	Ramani za upimaji zimeandaliwa bado kupelekwa wizarani.

3. Kitengo cha Uthamini

NA	MRADI/SHUGHULI	UTEKELEZAJI	MAELEZO
1.	Kukadiria viwango vya kodi za ardhi kwa wamiliki wapya na wale wa zamani.	Jumla ya viwanja 161 vimekadiriwa kodi na kuwasilishwa kwa wamiliki.	Zoezi linaendelea.

4. Kitengo cha Ardhi.

NA	MRADI/SHUGHULI	UTEKELEZAJI	MAELEZO
1.	Kuandaa hati kwa wamiliki wapya wa viwanja.	Jumla ya hati miliki 80 zimeandaliwa.	Hati 67, zimewasilishwa kwa Kamishina wa Ardhi kanda ya Tabora kwa kuidhinishwa.Hati 13 wateja hawajakamilisha malipo yao.
2.	Kusimamia uhamishaji miliki za ardhi za wananchi.	Jumla ya wananchi 22 wamewasilisha maombi ya kuhamisha miliki zao.	Maombi yote yametekelezwa.
3.	Kupokea, kusikiliza na kutatua migogoro ya Ardhi.	Jumlaya ya migogoro 17 imeripotiwa, na tunaendelea kuishughulikia ikiwa ni pamoja na: i. Mgogoro wa wananchi wa kata ya Luhita na chuo cha Mubondo. ii. Mgogoro uliopo kata ya Mganza kati ya wananchi na Ndugu Aldof Mfumya. iii. Migogoro iliyopo kata ya Muhunga kati ya Shirika la tumbaku na wananchi.	Kati ya migogoro hii 17, migogoro 11 imetatuliwa na migogoro sita(6) ipo katika hatua mbalimbali za utatuzi.
4	Ugawaji wa viwanja eneo la Mtundu - Kabanga	Jumla ya viwanja 350 vimegawiwa kwa wananchi walioomba.	Taarifa ya mgao wa viwanja imesha wafikia waombaji wote waliopata.

5. Kitengo cha Maliasili.

N A	MRADI/SHUGHULI	UTEKELEZAJI	MAELEZO
1.	Ugawaji wa miche	Jumla ya miche ya miti ya miyovu 11428 imegawiwa katika Kata tano(5) na Taasisi za Elimu tatu(3). Heru juu miche 1000, Mganza miche 100, Msambara miche 1000 Kanazi miche 1628 na Nyasha miche 1800, jumla miche 6428. Pia tumegawa jumla ya miche 5000 kwa shule ya sekondari Muhunga, shule ya msingi Kamkata na shule ya msingi Uhuru.	zoezi hili ni zoezi endelevu.

- Kamati ilijadili na kuridhia vibanda vilivyoopo kwenye geti la Hospitali ya Mlimani wapewe maeneo karibu na bohari ya Elimu ya zamani ili biashara zao ziendee pale na kuepusha usalama wao na mali zao .

KUWASILISHA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA IDARA YA USAFI NA MAZINGIRA KWA KIPINDI CHA JANUARI - MACHI 2017

MH.MWENYEKITI

Katika kipindi cha robo ya tatu yaani Januari –machi 2017 Idara ya usafi na mazingira ilifanya shughuli zifuatazo:-

1. Kutembelea kaya hadi kaya kukagua usafi wa mazingira katika mitaa 108 ya Halmashauri ya mji .Matokeo yalikuwa kama ifuatavyo kaya

zilizotembelewa 26,419 ,Idadi ya vuoo vya asili 15381(58%) vyoo vya asili vilivyoboreshwa 3484(13%) vyoo vyenye bomba la kutoa hewa VIP) 1986(7.5%) Vyoo vya maji 2262(8.6%) hakuna choo 2606 sawa (25.9).

2. Ukaguzi wa majengo ya biashara migahawa 13, virabu vya pombe 20, Baa 15 Mashine z a kusaga nafaka 176, bucha 18, masoko 6, machinjio 3, Nyumba za kulala wageni 86 saluni 110, mamalishe 78 na nyumba za sinema 8 wote walipewa ilani ya kurekebisha kasoro zao na kutekeleza ndani ya muda

3. Ukusanyaji nausafirishaji wa taka taka zilizokusanywa kwenye vizimba vya ofya , Bogwe,Bucha – Murusi, Mwilamvya na Mnarani na kuzolewa kwa kutumia trekta na gari la kukodi (Tipper)

4. Ukaguzi wa mazingira ya vyanzo vya maji Balaza la Taifa la hifadhi ya mazingira (NEMC) kwa kusaidiana na mamlaka ya maji mjini (KUWASA) na Idara ya Mipango miji walitembelea vyanzo vote vya maji Ksulu Mjini. Mapungufu yaliyobainika ni kilimo kinachofanyika karibu na vyanzo vya maji, kuchimba mchanga na kuopoa kokoto ndani ya chanzo ,Ujenzi karibu na chanzo.

   Aidha walibaini matatizo hayo na kuahidi kwenda kuyafanyia kazi .

5. Kutoa elimu ya hifadhi ya mazingira katika kata ya kimobwa. Elimu ilitolewa ya kutunza vyanzo vya maji hususan chanzo cha Nayenge wananchi walielimishwa madhara ya kulima karibu na vyanzo na kujenga karibu na vyanzo.

6. Upandaji miti kwenye vyanzo vya maji miche ya miti aina ya minyovu ilisambazwa Heru juu – Miche 1000, Muganza miche 1000, Msambara Miche 1000, Kanazi miche 1628, Nyansha 1800, Jumla ya miche ilikuwa 6428.

Naomba kuwasilisha.